



**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA
MITAA**



HALMASHAURI YA WILAYA YA MVOMERO

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. MVDC/L.10/ 1VOL.I/97

Tarehe 21.08.2023

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero anatangaza nafasi za kazi za Ajira ya Mkatoba kwa nafasi ifuatayo;

1. Msaidizi wa Hesabu Daraja la II Nafasi 4

SIFA ZA MUOMBAJI

Kuajiriwa wenye Cheti cha Astashahada ya Uhasibu kutoka Chuo kinachotambulika na Serikali au Cheti cha ATEC I kinachotolewa na NBAA au sifa nyingine zinazilingana na hizo zinazotambulika na NBAA.

MAJUKUMU YA KAZI

- I. Kuandika na kutunza " Register " zinazohusu shughuli za Uhasibu.
- II. Kutunza kumbukumbu za Hesabu.
- III. Kupeleka barua / nyaraka za Uhasibu Benki.
- IV. Kufanya kazi zingine za fani yake atakazo pangwiwa na Mkuu wake wa Kazi.

Ngazi ya Mshahara TGS B

MASHARTI YA UJUMLA

- a) Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45 na usiopungua miaka 18.
- b) Waombaji wote waambatanishe vyeti vya kuzaliwa na passport size 2 za hivi karibuni.
- c) Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi (CV) yanayojitosheleza yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (3) wa kuaminika.
- d) Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma nakala za vyeti vya Kidato cha IV na Kidato cha VI, vyeti vya kuhitimu mafunzo kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
- e) Hati za matokeo ya Kidato cha IV na VI havitakubalika.

Maombi yote yatumwe kwa;
Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero,
S.L.P 663,
MOROGORO.

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 04.09.2023 saa 9:30 mchana.

Limetolewa na ;

Linno P. Mwageni
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
MVOMERO

